# CHUO KIKUU CHA GARISSA

## MTIHANI WA MWISHO WA SEMISTA

Idara ya **Sanaa na Sayansi ya Kijamii**
Shahada ya **Elimu (B.Ed-Arts)**
Semista ya **Pili 2017/2018**
**EDK 216: Mbinu za Kufundisha Kiswahili I**
Muda: **Saa 2**
Tarehe:**10/4/2018**
Mkondo**: School Based**

**Maelekezo:** Jibu swali la **KWANZA** na maswali mengine **MATATU**
Swali la **KWANZA** ni la **LAZIMA**

---

1. (a). Fafanua vipengele vyovyote VITANO vya Nadharia ya Ufundishaji kwa vitendo inayotumiwa kufundisha lugha ya pili. **(Alama 5)**

   (b). Eleza jinsi utakavyotumia mbinu ya kazi-mradi kufundisha somo la fasihi simulizi kwa wanafunzi wa kidato cha tatu. **(Alama 10)**

   (c). Jadili changamoto zozote TANO zinazotokana na hali ya wingilugha nchini Kenya. **(Alama 10)**

2. (a). Jadili malengo yoyote MATANO ya elimu ya sekondari nchini Kenya. **(Alama 5)**

   (b). Eleza kwa mifano mwafaka umuhimu wa kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. **(Alama 10)**

3. (a). Kwa kuzingatia hoja zozote TANO onyesha tofauti za kimsingi zilizopo baina ya lengo la jumla na lengo mahsusi. **(Alama 5)**

   (b). Andaa maazimio ya kazi yatakayokuwezesha kufundisha somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha pili kwa muda wa wiki moja. **(Alama 10)**